



SHERIA ZA MIRATHI NA WOSIA TANZANIA

MASWALI

1. Nini maana ya Wosia?

JIBU

Wosia ni kauli au maandishi anayotoa mtu kuhusu namna angependa mali yake igawanye pindi atapofariki.

2. Kuna aina ngapi za Wosia?

JIBU

zipo aina mbili za Wosia ambazo ni,

- Wosia wa Mdomo
- Wosia wa Maandishi.

Wosia wa mdomo ni wosia unaotolewa kwa njia ya kauli na si maandishi. Pia wosia wa mdomo unatakiwa kutolewa mbele ya mashahidi wasiopunguwa wane.wawili kati ya wanne wawe ndugu wa mtoa wosia wengine wanaweza kuwa watu baki.

Wosia wa maandishi wa maandishi unatolewa kwa njia ya maandishi na si kauli.

3. Je ni vigezo vipi ambavyo anatakiwa awe navyo mtoa wosia?

JIBU

(i) Awe na akili timamu.

(ii) Awe na umri wa miaka 18

4. Vitu vipi vya Msingi vya Kuzingatia wakati wa kutoa wosia?



JIBU

Kwa wosia wa mdomo lazima mashahidi wote wanne wawepo kwa wakati mmoja, pia mrithi hawezi kuwa shahidi wa mtoa wosia.

Kwa wosia wa maandishi unapaswa kutolewa mbele ya mashahidi wasiopungua wawili, pia kwa mwosia asiyejua kusoma lazima awe na mashahidi wasiopungua wanne, wosia uandikwe kwa karamu ya wino na si risasi.

5. Je kuna Athari zipi mkutano wa ukoo kutofanyika ili kuweza kufungua Mirathi?

JIBU

Athari inayoweza kutokea baada ya wajumbe kutofanya kikao cha ukoo ni kukosekana muhtasari ili kuweza kufungua Mirathi, hivyo kupelekea ugumu katikakufungua Mirathi.

6. Je Msimamizi wa Mirathi ana Haki zipi na wajibu kisheria?

JIBU

Msimamizi wa mirathi atakuwa na haki na wajibu kama ifuatavyo:-

1. Kukusanya madeni ya Marehemu.
2. Kutoa fedha kwa ajili ya gharama za mazishi.
 - Kugawa mali za Marehemu kwa warithi waliobinishwa.
1. Kutojinufaisha na mali za Marehemu.
2. Kushitaki kuhusu suala lolote kama ambavyo angefanya Marehemu kabla ya kifo chake.
3. Je utaratibu upi hufuatwa katika kulipa Madeni ya Marehemu?

JIBU

Sheria ya Urithi na usimamizi wa mirathi inabainisha namna ambavyo madeni ya Marehemu yanatakiwa kulipwa kama ifuatavyo:-

- (i) Gharama za mazishi na gharama za matibabu.
- (ii) Malipo kwa huduma zilizotolewa kwa maehemu na mfanyakazi au Kibarua nk.
- (iii) Gharama za ufunguzi na usimamizi wa Mirathi.



(iv)Malipo ya madeni mengine yaliyoachwa na Marehemu.

8.Je ni utaratibu upi hufuatwa katika kufungua Mirathi?

JIBU

(a)KAMA MAREHEMU AMEACHA WOSIA

(a)Kifo kiandikishwe katika ofisi ya Vizazi na vifo katika wilaya ambayo kifo kimetokea, kisheria muda wa kuandikisha ni siku 30 baada ya kifo kutokea.

(b)Msimamizi aliyeteuliwa na Marehemu katika wosia ndiye mwenye mamlaka ya kufungua Shauri la mirathi katika Mahakama husika.

(c)Kama wosia haujataja msimamizi wa mirathi utaratibu utahitaji kikao cha ukoo kikae na kupendekeza jina au majina ya wasimamizi wa Mirathi.

(d)Mahakama baada ya kupokea maombi ya usimamizi wa mirathi.Mahakama itatoa utaratibu wa muombajikughaamia tangazo la mirathi kwenye gazeti pia tangazo litatoa iku 90 kuruhusu pingamizi.

(e)Mahakama itamruhusu Msimamizi wa Mirathialiyeteuliwa kugawa mali za marehemu kulingana na wosia.

(b) KAMA MAREHEMU HAKUACHA WOSIA

(a)Kifo kiandikishwe katika ofisi ya Vizazi na vifo katika wilaya ambayo kifo kimetokea, kisheria muda wa kuandikisha ni siku 30 baada ya kifo kutokea.

(b)Mkutano wa ukoo ukae na kupendekeza jina au majina ya wasimamizi wa mirathi.

(c)Mahakama ikishapokea maombi ya usimamizi wa Mirathi itatoa utaratibu kwa muombaji kugharamia tangazo la Mirathi kwenye gazeti. Tangazo litatoa muda wa siku 90 kuruhusu Pingamizi.

(d) Msimamizi atawajibika kugawa mali za Marehemu kwa warithi kulingana na Sheria.



9. Je ni taarifa zipi Muhimu katika Shauri la Mirathi?

JIBU

- (i) Cheti cha kifo
- (ii) Nakala ya Muhtasari wa kikao Cha ukoo.
- (iii) Majina ya warithi halali wa mali za Marehemu
- (iv) Vyeti vya kuzaliwa vya watoto
- (v) Nakala ya Wosia kama marehemu aliacha wosia.